# CHAMA CHA WANAWAKE WACHIMBA MADINI TANZANIA

# MABADILIKO YANAHITAJIKA ILI KUWAWEZESHA NA KUONGEZA IDADI YA WACHIMBAJI WADOGO WADOGO

Tanzania inashika nafasi ya juu kwa kuwa na hazina kubwa ya madini barani Afrika. Sekta ya madini ndio inayokua kwa kasi katika kuongeza pato la taifa la Tanzania, na ndio inayochangia karibia nusu ya mauzo yasafirishwayo nje ya nchi.

Tanzania ni miongoni mwa nchi masikini sana duniani, lakini ina hazina kubwa ya madini ya dhahabu yenye thamani zaidi ya dola za kimarekani billion 39, na madini mengine yanayodhaniwa kuwa na thamani kubwa zaidi ya hiyo. Mabadiliko ya sheria ya madini yaliyofanywa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita ilisaidia shughuli mbalimbali za uwekezaji mkubwa kwa kupitia wafanyakazi wa sekta ndogo ndogo. Sera, sheria na kanuni hizo hizo zilizokuwepo hazikuwasaidia wachimbaji wadogo wala wanawake.

Aidha, mfumo wa utoaji leseni wa sasa umewatenga wachimbaji wadogo huku ushiriki wa wanawake katika sekta hiyo ya madini ukiwa ni mdogo na upo katika ngazi ya chini sana.

Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inampa Waziri wa Nishati na Madini mamlaka zaidi ya kutengeneza kanuni kwa ajili ya sekta hiyo. Kwa sasa kuna kanuni 13 zilizoanzishwa na Wizara hiyo, na katika hizo hakuna hata kanuni moja inayozungumzia moja kwa moja hali ya biashara ya wachimbaji wadogo. Kanuni za sasa za madini pia zimeongeza ugumu kwa wachimbaji wadogo katika kupata leseni chini ya mfumo mpya wa zabuni uliopo.

Chama cha Wanawake wachimba Madini Tanzania (TAWOMA), kinahamasisha ushirikishwaji mkubwa wa wachimbaji wadogo pamoja na wanawake waliopo katika sekta ndogo ndogo za maendeleo ya madini kwa kuwashirikisha kwenye utungaji wa sera na sheria za sekta hiyo.



Wanawake zaidi ya 300,000 wameajiriwa katika sekta ya madini

- Theluthi mbili ya shughuli zote za madini nchini Tanzania inamilikiwa na makampuni makubwa ya kimataifa ya AngloGold Ashanti na Barrick Gold.
- Takribani ajira milioni 3 zilizalishwa na wachimbaji wadogo, huku makampuni makubwa ya uchimbaji wa madini yakizalisha ajira 500,000 tu hadi kufikia mwaka 2011.
- Inakadiriwa kuwa wanawake 300,000 wameajirwa katika sekta ya uchimbaji wa madini.

### WACHIMBAJI WADOGO WANA HAKI NDOGO SANA IKILINGANISHWA NA ILE WALIYONAYO WACHIMBAJI WAKUBWA - SOMO YAKINIFU -

Mathalani, mchimbaji mdogo amegundua dhahabu shambani. Ili aweze kupata leseni ya awali ya uchimbaji (Primary Mining License) mchimbaji huyo lazima afuate hatua zipatazo kumi, kabla hajaanza kazi ya uchimbaji; mlolongo ambao huenda ukamchukua hadi mwaka mzima.

Mwombaji huyo atatambulika kuwa mchimbaji halali wa madini pale tu maombi yake yatakapothibitishwa na Ofisa Madini wa Kanda.

Kwa upande mwingine, Waziri ana mamlaka ya kutoa leseni inayotazamiwa (Prospective License-PL) ndani ya muda mfupi kwa wachimbaji wakubwa.

Aina hii ya leseni (PL) inatoa haki ya kuwa na maeneo makubwa ya ardhi vikiwemo vijiji na maeneo mengine ambayo tayari yameshatengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Wakati mchimbaji mdogo anatakiwa kuwa na kibali kutoka kwa uongozi wa kijiji kwa ajili ya kupata leseni ya awali ya uchimbaji wa madini, wachimbaji wakubwa hawana haja ya kuwa na utambulisho huo. Kwa mujibu wa sheria ya madini, ardhi ni mali ya serikali ya kijiji, lakini madini yaliyomo ndani ya ardhi hiyo ni mali ya serikali kuu.

## MADAI YA WACHIMBAJI WADOGO:

### MABADILIKO YA SERA:

- Kuwepo na mfumo rahisi na wa wazi wa utoaji leseni.
- Maombi ya leseni yafanyike katika ngazi ya wilaya katika maeneo yote ya uchimbaji wa madini.
- Kusiwe na uthibitisho unaohitajika kutoka kwa waziri kwa ajili ya kupata leseni ya uchimbaji mdogo mdogo.
- Kuwepo na kanuni maalumu za usimamizi wa mazingira zinazofaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo tu.
- Kutambuliwa kwa uchimbaji mdogo mdogo kama sehemu muhimu inayochangia pato la taifa.
- Kuwepo na mamlaka moja ya utoaji wa vibali kwa uchimbaji mdogo mdogo wa madini.
- Kuanzishwa kwa idara au kitengo maalumu kitakachoshughulikia masuala ya uchimbaji mdogo mdogo wa madini.

### MABADILIKO YA SHERIA YA MADINI:

- Kuwepo na kanuni zilizowazi za umiliki na utumiaji wa ardhi na madini.
- Mchakato wa maombi ukamilike ndani ya kipindi cha wiki mbili hadi nne.
- Sheria iweke wazi vifungu vinavyowahusu wachimbaji wadogo na wale wa vito vya thamani.
- Sheria zilizopo zisaidie wachimbaji wadogo
- Kuwepo na haki sawa kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa
- Sheria iruhusu umiliki wa eneo kubwa na mkataba wa muda mrefu.
- Sheria iruhusu uhamishaji na uwekaji rehani wa haki ya uchimbaji wa madini.
- Sheria itenge baadhi ya maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo mdogo wa madini
- Sheria inatakiwa ishughulikie malengo yote yaliyojitokeza katika sera ya madini ya mwaka 2009.

FACT SHEETS for ACTION

This Fact Sheet was prepared with assistance from Pamoma Limited.
Published on 20 June 2012.

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy